

# KIRANGA KOMO

Muddyb Mwanaharakati

FANANI MPOLE

Kimechapwa na,  
Fanani Mpole,  
Dar es Salaam,  
Tanzania.  
Mob: 0654-846-084.

Mhariri: Eric Gamba  
Msanifu kurasa: Muddyb Mwanaharakati  
Jalada: John Wisse

**ISBN: 978-9976-5467-3-6**

© Muddyb Mwanaharakati, 2020  
Mobile: 0713538427  
Chapa ya kwanza, 2020

Haki zote zimehifadhiwa.  
Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kuuza, kupiga chapa, au kukitoa kitabu hiki  
kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya kimaandishi kutoka kwa Muddyb  
Mwanaharakati.

**TABARUKU**

*Kwa wawulana na wasichana wote,  
Zingatieni nasihi za waliona mizunguko mingi ya jua la dunia yetu.*

## SHUKRANI

Sina mengi ninayoweza kuyaandika juu ya shukrani zangu kwa Mola wangu. Hasa kwa kunipa kipawa hiki cha uandishi wa riwaya. Mama yangu mzazi, Rehema Mohamed Ali. Siwachi na wala sitowacha kukutaja katika kila kitabu changu nitakachoandika. Nina nini mimi bila ya wewe? Nakukumbuka kila iitwayo leo. Huko uliko Mungu akupe kauli thabiti.

Mke wangu kipenzi, Advera – Mama’ke Ibrahim, Haytham na Ilham. Ninakupenda mno. Zaidi kwa kuniamsha asubuhi ili niendeleo kuandika riwaya hii na nyengine nyingi tu. Mungu ametuleta pamoja ili tuweze kuyafikia malengo yetu kama familia. Shukrani sana!

Shukrani za kipekee zimwendee kaka Eric Gamba kwa kukubali kuhariri muswada huu ukiwa katika umbo lake changa. Nimejifunza mengi kupitia wewe. Hakika wewe ni hazina tosha kwa vijana wa rika letu. Umejawa na mengi ya kuwafunza vijana wenzako.

Ahsante sana jirani yangu wa zamani, Mama Leila kwa kusoma kitabu hiki mwanzoni kabisa huku tukicheka na kufurahi. Shukrani sana Janyl Kimoto, Nawal Khaflan, Dina, Edna Ed, kaka Kevin Mponda na Japhet Nyang’oro kwa kuruhusu riwaya hii itumwe katika makundi yenu sogozi ya WhatsApp. Mzee Merinyo kwa kuthibitisha Uswahili mwingi umetumika humu. Kauli yako iliwasha cheche ya kupambana zaidi katika kuimaliza riwaya hii.

Shukrani wanachama wote wa **READING MARATHON** kwa mchango wenu wa hali na mali. Ninawapenda sana.

Mohamed O. Lupinga (Muddyb),  
Chanika, Ilala, DSM,  
19/10/2020.

Saa nne na dakika thelathini na tano usiku.

# KIRANGA KOMO



## SEHEMU YA KWANZA

**G**ari na pikipiki zilipishana kwa kasi huku zikipiga honi bila mpangilio maalumu. Hilo lilisababishwa na uwembamba wa barabara ya mtaa wa Dei Masoko, Kiwalani, Ilala – Dar es Salaam. Eneo lote limetapakaa vumbi kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara.

Hilo dogo, kubwa ni suala la wenyeji wa eneo hilo kushinda katika kijiwe cha kahawa kinachopakana na soko kubwa la Geza Ulole. Soko limejaaliwa tope jeusi linalotibua nafsi kwa kulitazama tu – wachilia mbali kuligusa. Harufu mbaya ya uozo wa masalia yaliyotupwa kando ya soko, kukazuka jaa lilisilo rasmi katika eneo hilo, likazidisha ukakasi. Hakuna mapumziko ya pua.

Kila wakati kidole juu ya mwamba pua.

Ajabu iliyopo, wenyeji hawasikii harufu hiyo. Hawana habari kila uchao wapo kijiweni kando ya soko. Vijana kwa wazee huketi wakichapa maongezi ya kusukuma siku. Ilikuwa saa nne asubuhi, nyakati za akina mama kwenda masokoni kupata mahitaji yao ya kila siku kwa ajili ya familia. Kando ya soko, kuna ujia unaotokea barabara kuu ya Viwandani – Vingunguti. Kulikuwa na mwanamama mrembo kweli. Mwenye papi pana za midomo, jicho la kisu, umbo la tikiti maji, mteke mno mwili wake. Akitembea, ukanyagaji wake ardhi kama anaionea huruma. Uturi alioupiga ulituma salamu hadi kijiweni. Ukazua nadhari yao kutazama upande huo.

“Mmmhh! Mrs. Ticha huyo anakuja. Nausikia uturi wake,” alisema kijana mmoja. Jina maarufu Panga la Mwingireza – linakata kotekote. “Polepole babu, mumewe si unamjua kama baharia wa kutupwa?” alijibu mtu mzima mmoja hivi huku akisogeza kete yake katika drafti walilokuwa wakicheza kijiweni hapo.

“Tulia we mzee. Em fanya yako huko,” Panga alijibu. “Ayaa!” babu akalalama. Katumia mbinu mbaya kumdhibiti mbaya wake katika drafti.

“Panga nisaidie basi!” babu aliomba msaada wa Panga. Vijana wakacheka. “Panga hawezi kukuelewa kwa sasa. Hadi Mrs. Ticha akisepa—pengine atakuelewa,” alisema kijana wa kando ya babu.

Panga mdomo wazi akimtazama mrembo huyo. Mungu bariki mke wa Ticha akapita walipo.

“Habari zenu!” alisalimia mke wa Ticha huku akiwapungia mkono. “Nzuri tu, shemegi—karibu sana bana!” alijibu Panga la Mwingereza. *Upesiupesi* utasema salamu ile ilimhusu pekeye. Hakuridhika kupora salamu ya kijiwe kizima, akatupia na tabasamu. Kama haitoshi, akamminya na kijicho kidogo, akatua kwa tabasamu la kifedhuli.

Mrs. Ticha alitambua hila ya Panga. Akatapika neno.

“Afu Panga—jiangalie. Ohooo! N’tamwambia mzee wangu akufanyishie ujuwe!” mke wa Ticha alitishia. Panga akacheka. “Aah wapi! Mtishie nyau, mi’ mtu mzima utaniweza wapi?” Panga alijibu. Mke wa Ticha akacheka. Hakusimama. Aliendelea na safari zake.

Alienda kugota katika meza ya mwuza samaki wabichi. Jicho la Panga halikusita kutupwa mpaka kule alipo mke wa Ticha. “Dah!” alisikitika Panga huku akimwanguka mke wa Ticha.

“Kijana, tushakwambia sisi tayari. Huo sio mwendo mzuri kabisa!” alisihi mzee mmoja kijiweni hapo. “Sijafanya kitu lakini, mzee wangu,” Panga alijitetea. “Majuto ni mjukuu, mdogo wangu!” aliongeza mzee huyo. Panga hakusikia la mwadhini wala mnadi swala.

“Naona unanikomesha kwa vile ushapigwa tayari. Kisa sijatoa *support* tena nd’o unaingilia mipango yangu!” Panga alijibu kwa kebehi huku akigeuza jicho lake katika drafti. Kimya kikazuka. Wote walizingatia zaidi mchezo uliokuwa ukiendelea.

“*Moyo hausemezeki, kwa kile ukipendacho!*” aliimba Panga wimbo wa Abdallah Issa. Jamii ilimsikia akinadi mapenzi kwa mali ya mtu. Wapo waliosikitika na wapo waliofurahishwa na hilo. Panga hakujali maneno yao.

\*\*\*\*\*



Asubuhi siku iliyofuata, ilikuwa Jumapili. Hakuna kazi. Panga aliamka majira ya saa moja na robo asubuhi. Kwa uchovu, akajinyoosha, akatoka nje akiwa na boksa nyepesi ya mpira. Kifua wazi, akafungua mlango wake wa chumba cha uani – ubavuni.

Hamadi! Chumba cha pili alisimama mke wa Ticha. Alikuwa akigonga mlango ufunguliwe. “Shoga, bado tu hadi mida hii huko kuridhishana? Aaah, jamani! Mtamalizia baadaye. Em nifunguliege huko mie!” alisema mke wa Ticha. Akaamsha tabasamu baada ya kumuona Panga kifua wazi huku via vya uzazi vikionesha kuwa hai.

Akarudi ndani upesi kwenda kujisitiri zaidi. Akatoka baada ya kuvaa suruali na shati jepesi lisilo na mambo mengi. “Mbona umekimbilia kwenda kuvaa nguo tena? Unaniogopa eh?” alisema mke Ticha huku akitoa tabasamu.

“Hapana!”

“Kumbe je?”

“Ninakuheshimu tu, wewe!”

“Eti eh?”

“Ndiyo, mama Ticha!”

“Sikubaliani na maneno yako!”

“Ukweli haujawahi kukubaliwa na jamii kirahisi.”

“Wacha maneno yako!”

“Kweli, mama Ticha.”

“Na cha jana je?”

“Kipi hicho?”

“Kunitumbulia macho kila nikanyagapo!”

“Ilikuwa zuga tu kufurahisha baraza pale kijiweni!”

“Nyoo. Yatakushinda. Mtoto mdogo – kutaka gari kubwa!”

“Mtoto hiyo una kadi langu weye?”

Kabla mama Ticha hajajibu, mlango ukafunguliwa aliokuwa akiugonga. “Vipi hivyo mwenzetu? Mpaka mida hii?” mama Ticha alimaka.

“Bibi wee! Kwani unanisaidia kulipa kodi hapa?” mama Ashura alifoka. Ni baada ya kuamshwa asubuhi na mapema.

“Eeh, jamani! Kama umezidi tusiseme?”

“Wacha leja, mwanamke. Sema shida yako. Kipi kilichokuleta asubuhi hii,” mama Ashura aliendelea kufoka. Hakutoa fursa ya kuchunguzwa na mke wa Ticha. Mama Ticha akakubali yeshe.

“Shoga, sio kwa kunikomesha huko!” alisema mama Ticha huku akirudi nyuma hatua moja. Akamvuta mkono mama Ashura na kasogea kando kidogo. Wakiwa katikati ya maongezi, Panga akapita. Akamwamkia mama Ashura.

“Ma’ Ashura – shikamoo!”

“Marhaba, mdogo wangu. ‘Ujambo?’”

“Sijambo, dada!” Panga alijibu. Akapita zake kuelekea chumbani kwake. Vyumba vyao vya ubavuni. Waliposimama ni uchochoro baina ya vyumba na ukuta wa nyumba kubwa. Nayo ina wapangaji rundo. Mama Ticha alisema shida yake, kisha akarudi nyumbani kwake.

Panga alitoka baada ya saa zima la kubaki chumbani kwake. Chumba cha msela. Jiko la Mchina, sifuria tatu, moja ya mboga, moja ya ugali, nyingine ya chai. Ndoo ndogo za maju ya kunywa na kuogea.

Vikombe vya kuhesabika. Haivuki vitatu. Kikopo cha sukari, sahani tatu, bakuli tatu. Kibeseni kidogo cha kuwekea vyombo. Kitanda cha boksi, yaani chini hakuna uvungu. Kimezibwa. Shuka tatu, mito miwili – japo kila siku hulala pekeye. Wakati wa mechi za msimu, ndiyo hutumiwa.

“Una nini kaka’ke!” alisema mama Ashura huku akimgongeshea mkono Panga. Panga akarejesha gongesho huku akijiweka sawa. Uso wake ulieleza yote kama ana jambo moyoni. “Em tapika nyongo nikusikie kwanza, kijana!” alisema mama Ashura. Akatua na tabasamu hafifu.

“Dah!” alisema Panga huku akiweka sawa shati lake. Alivalia raba nyeupe na suruali nyeusi. Juu shati leupe alilozubaisha na singlendi kwa ndani. “Kusema ukweli, dada!” alisema Panga kisha akatua. Kimya kikatawala. Akamtazama usoni mama Ashura.

“Sema bwana – unapoteza muda wangu!” mama Ashura alimaka. “Si kuhusu yule mtu, ma’ Ashura bwana!” Panga akatapika nyongo. “Nyoo! Nilijua tu! Maana si kwa jicho lile ulilokuwa ukilitua kila ulipopita tukiwa tumesimama!” mama Ashura alichagiza. Panga akacheka.

“Kinacho-kuchekesha?” mama Ashura aliuliza. “Amna kitu bana!” Panga alijibu. “Nikwambie tu, yale maji mazito. Wameshindwa watu pale. Unachokitafuta, utakipata!” alisema mama Ashura. Dhahiri kauli hiyo haikufanya kazi kwa Panga.

“Watu gani sasa?”

“Watu, watu. We’ ulitaka watu gani?”

“Si ana mume yule?”

“Naye jicho linamtoka. Seuze we’ mburu matari?”

“Aaah, mama Ashura!”

“Nimefanyaje?”

“Mbona unanifanyia hiyana?”

“Nikufanyie hiyana mie?”

“Ndiyo!”

“Kwa lipi?”

“Hilo-hilo!”

“Kwani unasemaje, Panga?”

“Mi’ nataka unifanyie koneksheni!”

“Heee! Makubwa!”

“Makubwa gani, mama Ashura bana!”

“We’ mtoto we’!”

“Mi’ sio mtoto!”

“Na ukubwa pia huna!” Panga akakwazika na vikwazo alivyoweka mama Ashura. Akasahau kila mchuma janga hula na wa kwao. “Sikuelewi, mama Ashura,” Panga alimaka. Mama Ashura akatikisa kichwa.

“Kwa hiyo unataka mi’ nifanyeje?” mama Ashura aliuliza. “Si’ n’shasema? Niungie pale!” Panga alijibu. Mama Ashura akaonekana kuingia

katika tafakuri nzito. “Naona umeyachoka marinda yako!” mama Ashura alisema. Panga akakunja uso.

“Basi mdogo wangu –ha ha ha ha!” mama Ashura alijichekesha. Ni baada ya kuona sura ya Panga imebadilika. Panga akachuma tabasamu.

\*\*\*\*\*

Salamu si mzigo, kusema kwamba kuzipeleka utahitaji guta au usafiri kuzifikisha kwa mlengwa. Jioni majira ya saa kumi na moja, kibarazani katika nyumba ya Biti Nyampeta –kuliketi wamama wengi wakitazama wapita njia waliokuwa wakienda na wengine wakirudi.

Kwa watu wa ukanda wa Uswahilini ni jambo la kawaida nyakati za jioni akina mama kukaa vibarazani. Kila anayepita atachambuliwa hadi rangi ya nguo ya ndani aliovaa. Miguu, mwendo, sura, nguo, kama ana bwana au mabwana wote watatajwa.

Ilikuwa jioni tena, jua lilikuwa linazama, kwa mbali alionekana mama Ashura akija eneo la nyumba hiyo. “Karibu, shosti!” alisema mama Ticha. Naye alikuwa sehemu ya wamama walioketi kibarazani. Mama Ashura tena hakusubiri amaliziwe kauli, kwamba kaa chini.

Akajitupa mkekani, puu. Akajiweka mbele ya mama Ticha –mapajani kwake akiegemea mgongo. Wale wamama wakacheka. “Mama Ashura una vituko! Jamani!” alisema mama wa pembeni yake. Winga ya kulia. Kwa sauti ya chini sana, mama Ashura akasema.

“Salamu si mzigo,” alisema mama Ashura, akasita kuendelea. Akawatazama wanawake wa pembeni, je, wamezingatia maongezi yao? Ndivyo ilivyokuwa!

“Si mwende chemba jamani kama mna lenu la siri?” yule mama alimaka. Wakajibeba mtu na shogaye, kando. Bado waliendelea kutumbuliwa macho na wale wakina mama. “Shosti, twende ndani. Kambi imevamiwa!” mama Ticha alisema. Wakati wanaingia ndani, nyuma vicheko vikatamalaki. “He he hee! Halooo!” Mtu na shogaye, hawakujali. Ni kawaida yao kila siku kuchimbana. Kusema watu na mambo yao. Waswahili na Uswahili wao.

Wakaingia sebuleni kwa mama Ticha. Sebule za Kiswahili zinafanana. Meza moja kati, kando kuna jiko la Mchina kwa ajili ya kupikia chai na ugali wa haraka. Mapishi makubwa nje, jikoni uani huko changanyikeni. Ukipikia ukumbini, unatafuta neno na mama mwenye nyumba. Atakuimba – kitongoji chote kitajua ulichokifanya.

Upenuni mwa sebule, kuna TV aina ya Panasonic na deki ya mkanda wa mkubwa. Imefunikwa na kitambaa cheupe chenye urembo wa maua ya rangi nyekundu. Seti ya kochi. Yaani, kochi la watu watatu na mbili za kujitegemea. Kuna dirisha mbili. Moja upande wa nyuma ya kochi kuu, lingine upande wa kushoto wa kochi kubwa ambapo ndipo kulipowekwa TV.

Hivyo mkitazama TV, mwanga pia unakumbana nao. Waliweka hivyo ili kupunguza mwanga wa nje usipige katika TV.

Wakajitupa katika kochi la watu watatu. Wakitazamana, maongezi yakaanza.

“Hivi unaishi nao vipi hawa viumbe?” mama Ashura aliuliza kidadisi huku jicho lake likimakinika kusubiri jibu la shogaye. “Sema shida’ko achana na wale malaya!” mama Ticha alimaka. Mama Ashura likamshuka, shuu!

“Shoga, nina salamu zako!”

“Salamu gani tena?”

“Salamu, salamu!”

“Kutoka kwa nani?” swali la mama Ticha likamtia ububu mama Ashura. Akainua kichwa kumtazama, mara akakirudisha chini. Kabla ya kusema hizo salamu. Mama Ticha akadabua ujio huo.

“Komaaaaa!” mama Ticha alijibu. “Loh! Ni mpeleke wapi mtoto mdogo kama yule? Kweli umenichoka, mama Ashura!” mama Ticha aliongeza. “Bibi weee! Em wacha leja kwanza,” alisema mama Ashura, akatua. “Una kadi lake la kiliniki hata umwite mtoto yule?” mama Ashura aliongeza.

“Tema mate chini, mama Ashura! Loh! Hapana kwa kweli!” alisema mama Ticha huku akikung’uta mikono. “Sina hamu!” aliongeza mama Ticha. “S’kia bibi kama wewe. Tarishi hauawi, madhali salamu zimefika, basi we utaamua kuula wa chuya au uuchambuwe!” alihitimisha mama Ashura.

“Nimekushindwa kwa kweli, mama Ashura! Khaa!” mama Ticha aliendelea kujibaraguza. “Jukumu langu limeisha. Kazi kwako tena! Mtodo kakuelewa yule. Tena kasema atakupata vitu tangu uzaliwe hujawahipo kuwaza!” mama Ashura alichombeza.

“Vitu gani hivyo sijawahi kuvipata na umri huu?” mama Ticha alisema. “Ohh, usiseme hivyo, jamani. Bibi kama wewe unaweza kujikuta umezama mzimamzima kwa kitoto kile ukaanza kulia unajuta kwanini ulichelewa kumfahamu!” mama Ashura alichagiza.

“Aaaah wapi! Si kwa namba hii wewe!”

“Nakwambia mimi sasa!”

“Kwanza ana umri gani yule? Nikimtazama hazidi miaka ishirini. Haya, nina thelathini na nne. Si mwanangu kabisa yule?”

“Wacha ubabaifu. Mwanao unamjuwa!”

“Nimetolea mfano tu!”

“Nd’o sio mwanao tena,”

“Mama Ashura, bwana!”

“Nd’o mie. Mwingine fotokopi!” Wakacheka hadi jino la mwisho.

## SEHEMU YA PILI

Sauti za malumbano zilikuwa za mnong’ono, pengine zingeweza kusikika kama ungepita karibu na dirisha. Mume na mke walikuwa katika malumbano mazito. Mume kashikwa ugoni. Mama Ticha kazifumana meseji za mapenzi kutoka kwa mwanamke mmoja aliyeseviwa jina la Mwashabani.

Neno limepata mnenaji.

“Kwa hiyo unadhani mi’ sitongozwi sio?” mama Ticha aliwaka. Mume akaingiwa na baridi. Mkunyato usio na majibu. “Nisamehe, mke wangu. Huyu mwanamke ni fitina tu. Ananitaka, mi’ simtaki!” Ticha alijitetea. “Weee! Weee! Usin’tie ujinga. Mtu anasema kabisa ‘*ahsante kwa shoo ya kibabe?*’” mama Ticha alifoka.

Ticha akamsogelea mkewe. Akamgusa begani. “Em niache mie,” mama Ticha alijebetua kibega chake huku akijisogeza mbali na mumewe. Mume akazidi kuwa mdogo. “Mke wangu!” mume alitoa neno. “Huyo mke unae we’ tu dunia nzima. Mke wangu, mke wangu – hebu nipishege huko,” mama Ticha aliendeleza nongwa lake.

Mume hakuongeza neno. Akatoka nje akiamuacha mkewe akiwa kafura mwili mzima. Pindi mume alivyotoka, mke akainua simu yake iliyokuwa juu ya droo la pembeni la kitanda. Akachakura nambari aliyokuwa akiitaka, akapiga.

“Eh, mama Ashura. Mwenzangu eh!” mama Ticha alisema na kuweka tuo. “Mwenzangu nini tena?” mama Ashura alidakia – ilisikika sauti yake kupitia spika za simu. “Si kaligalambua tena, baba Sudi!” alisema mama Ticha.

“Heee!” mama Ashura alitoa mshtuko.

“Eeeh, ndiyo hivyo!” mama Ticha alisema huku akijifuta mafua. “Sa’ nd’o unafanyaje ‘ivo?” mama Ashura alisema. “Mwenzangu hata sijui. Najionea tabu tu,” mama Ticha alisema. “Labda uende kwenu ukapumzike,”

mama Ashura alishauri. Mama Ticha hakujibu kitu. Badala yake, akatoa cheko dogo.

“Una wazimu kweli wewe,” mama Ticha alisema huku akicheka. “Sa’ wazimu huo veepee?” mama Ashura aliuliza. “Unataka nimkabidhi bucha fisi. Alinde nyama. Huyu dawa yake ni kupambana naye tu. Kamwaga ugali, mi’ namwaga mboga,” alisema mama Ticha. Mama Ashura akanyamaza kimya. Alikuwa akisikilizia mama Ticha ataongeza kitu gani.

“Umefilisika maneno, mama Ashura? Ah, sio kawaida yako!” mama Ticha aliongeza. “Hapana. N’nakusikiliza kwanza – urukeruke nione unatua wapi,” mama Ashura alijibu. “Jibu unalo,” mama Ticha alisema. “Kweli ninalo, lakini sio kwa kosa moja basi!” mama Ashura alisema akisikilizia majibu ya mama Ticha.

“Nani kakwambia moja? Nimeombwa msamaha mie mia mara inafika. Kila siku visanga. Naona sasa riziki yangu imetuwa. Wacha nimsabilie kitoto nione maajabu yake!” alisema mama Ticha. Mama Ashura huko aliko akaketi chini. Hakutaka kuamini kama maneno hayo yamepita katika ngoma zake za masikio yake.

“Hivi n’naota au namna gani?” mama ashura alisema. “Wala hauoti, shoga’ngu! Nimeamua sasa namimi nichachuke,” mama Ticha alisema. “Mmmhh! Mazito!” mama Ashura alisema. “Mazito kitu gani. We’ mbona unatembea na yule mwuza mkaa na watu tumekaa kimya?” mama Ticha alisema kwa hamaki.

“Nd’o ulipodondokea huko?” mama Ashura alisema kwa sauti ya kinyonge. “Eeh, tuulizane!” mama Ticha alijibu. “Haya, basi halalisha jambo lako. Usinitie mie katika uamuzi wako,” alisema mama Ashura huku akimsaili mama Ticha. “Ila,” alisema mama Ashura akanyamaza.

“Ila nini?” mama Ticha alihoji kwa kihoro.

“Kitoto kile kimekupania!” mama Ashura alisema akimfanyia kijicho mama Ticha kama vile anamuona wakati wangali mbalimbali. Wakazua kicheko cha kishambenga. “Wacha mtoto ajifaidie. Mi’ mwenyewe



n’shajichokea na maisha ya kuombwa misamaha kila uchao!” alisema mama Ticha.

“Basi tena, limepita hilo,” alisema mama Ashura na kukata simu.

\* \* \* \*

KATIKA vitu ambavyo mama Ashura hawezi kukaa navyo rohoni ni umbea na salamu za kikuadi. Ni kama moto ulioachwa chini ya kuni, wakati wa upepo unavuma, hakuweza kujizuaia kuwaka. Alitoka na furaha mno, baada ya kusikia mama Ticha kakubali ombi la kijana wake. Japo mwanzoni alijitia ubabaifu ati jambo la mama Ticha kumkubalia Panga ni ujinga wa kiwango cha lami. Akasahau kama yeye ndiye *tarishi* wa jambo hilo tangu hapo awali.

Mpangaji mwenzake. Mcheshi na msiri wake pia.

“Mbona kijuso kimejaa furaha— umeshinda BIKO Mshiko au?” Panga alimwuliza mama Ashura. Hakujiibu. Badala yake, akamshika mkono na kuketi naye kizingitini kwa Panga. “Otea kitu gani kimetokea?” mama Ashura alisema huku akichanua tabasamu.

“Bwana eh! Em niambie kitu gani?” Panga alimaka. “Kwani ulinituma kazi gani?” mama Ashura alisema huku akimwacha Panga atafakari mwenyewe. “Usiniambie bwana! Kakubali?” Panga aliruka kwa hamaki.

“Tenaaa! Chezea mimi we’” alisema mama Ashura. Kicheko. Wote kwa pamoja. “Nikajifanya kwanza kama namshangaa imekuwaje— mbona *ghafila-ghafila* namna hiyo. Nikamperemba sio vizuri mara vile, basi tu almuradi kumbabaisha. Mwishowe! Akabaki na msimamo wake,” alisema mama Ashura. Kicheko kidogo kikawa kimemshika.

“Dah!” Panga alisema.

“Dah— nini?” Mama Ashura akadakia.

“Siamini kilichotokea...”

“Nd’o uamini tena. Kazi yangu imeisha!”

“Aisee!”

“Nd’o ‘ivyo. Usimumize tu. Maana yule naye anajua kupenda,” mama Ashura alisema akifuata jasho. “Sitokuangusha, swahiba!” Panga alijibu kwa furaha. “Ila,” alisema mama Ashura. Akaweka tuo. “Ila nini tena, mama Ashura?” Panga alishtuka.

“Ha ha ha ha!” mama Ashura alicheka.

“Unacheka nini sasa?” Panga alimshangaa.

“Uyatunze marinda vizuri. Si unajua kama mke wa mtu ni sumu?” mama Ashura alisema huku akiendelea kucheka, kiganja mdomoni. Kaufunika. “Bwana we’ – potelea pote. N’shajivisha mabomu,” Panga alijibu kishujaa. “‘Aya twende – ‘tajua mwisho wake,” mama Ashura alijibu. Akaonekana kuzama mawazoni kidogo.

“Mbona kama umeduwaa hivi. Nini tena?” Panga alihoji.

“Kuna kitu kinaniumiza kichwa,” mama Ashura alisema akishusha pumzi. “Unajua yule mumewe ni malaya sana?” mama Ashura alisema. Akasita kuendelea. “Mbona huendelei tena?” Panga alihoji. “Moyo wangu. Unaogopa sana. Hofu wale huenda,” mama Ashura akasita tena. “Huenda nini, mama Ashura?” Panga aliwaka.

“Wale mambo mengi, Panga. Si mume, si mke. Hofu yangu umri wako na unapotaka kujiingiza. Lakini...” akasita tena mama Ashura. “Lakini nini, mama Ashura?” Panga aliendelea kuuliza kwa kihoro. “Kuna tetesi kwamba...” kabla hajamaliza, mume wa mama Ashura akatokea.

Maongezi yakafa. Panga akabaki na kihoro chake kinamtafuna kooni. “Hamjambo?” baba Ashura alisalimia. Hakushtuka na mkao aliomkuta mkewe akiwa na Panga. Anajua ukaribu wao na stori zao za vijiwani. Wakati mwingine hutazama pamoja tamthilia za Kihispania hadi nyakati za usiku – sebuleni kwa mama Ashura.

Panga akamwamkia baba Ashura, na kutoka.

\*\*\*\*\*

JIONI yake, walikutana. Panga na mama Ticha. Mkutano ulipanga na gwiji na fundi wa mipango wa mama Ashura. Ikawa siku ya kupeana mchakato mzima, matakwa ya mama Ticha kwa Panga.

“Sasa sikiliza – bwana kama wewe!” mama Ticha alisema, akasita kwa nukta chache. Panga hakutikisika. Alikuwa imara kusikiza maagizo. “Mimi nitakuwa wako. Lakini wako uliye naye usimwache kwa ajili yangu,” alisema mama Ticha, akanyamaza. “Enhee!” Panga alidakia. Mama Ticha akaendelea.

“Pili, nikikuhitaji – sitaki maneno mengi. Ni mwendo wa kufuata maagizo yangu. Unitoe mzigo wote. Sitaki mambo nusunusu, sijui nini, mara vile...” akanyamaza. Panga aliendelea kusikiliza.

“Tatu na mwisho, sitaki ubao wa matangazo. Mambo yangu ni mimi na wewe tu. Biashara ya kwenda kunitangazia kijiweni kwako pale Geza Ulole – sitaki!” mama Ticha alitua risala yake. Panga akashusha pumzi nzito. Mama Ticha akamtazama.

“Hakuna tabu!” Panga alijibu, akanyamaza.

“Nd’o maneno hayo tu?” mama Ticha aliuliza kwa kihoro.

“Mi’ kwako sina la kusema. Nitake nini zaidi ya kuwa karibu nawe? Niwachie mie. Nikuoneshe dunia ya kipekee. Dunia ambayo hukuwahipo kuipata. Bahari ya mapenzi ya kijana machachari!” Panga alijinadi.

“Maneno tu hayo. Tutaona hiyo siku,” mama Ticha alijibu kimashauzi. Panga akachekeka. Siku zikakatika. Panga alijitahidi sana kuitunza subira yake. Zaidi alihofia pupa pengine ingempeperusha ndege wake aliyeingia katika tundu bovu. Panga ni kipanga wa wanawake kama jinale la utani lilivyo.

Hakuwahi kuwa na subira katika suala la kupata mwanamke mpya. Hali ilikuwa tofauti kabisa kwa mama Ticha. Akili ilikubali kujiingiza kwa mwanamke ambaye mumewe ni dereva wa magari makubwa. Tena yale yenye safari ndefu.

Wengi kama si wote, huamini madereva wa malori kila kituo wana wanawake. Hilo huleta uwanja mkubwa wa kupata magonjwa ya zinaa kama si UKIMWI kabisa. Waliendeleza mahusiano yao kwa njia ya simu, ana kwa ana, vicheko na kadhalika.

Mapenzi yakapamba moto.

Siku moja isiyo na jina—mama Ticha alikuja wanguwangu kwa mama Ashura kuja kumpa taarifa juu ya alichokifanya mumewe. Mume akiwa chooni simu ikaita. Mke akaipokea, sauti ya kwanza, mwanamke! Maongezi yake na mama Ashura akimpa mkasa.

“Shoga, nimekuja!” mama Ticha alisema. “Haya, nini tena usiku huu wa saa mbili?” mama Ashura alishtuka. “Mwenzangu yule mume nimemchoka. Nimemchoka!” mama Ticha aliwaka. “Kafanyaje tena?” mama Ashura alihoji. “Kapiga mwanamke mwengine leo. Mbali na yule sijui Mwashabani!” mama Ticha alitapika nyongo.

“Loh! Makubwa!” mama Ashura alichagiza.

“N’naondoka leo!” mama Ticha aliendelea kuwaka.

“Usiondoke bibi we’!” mama Ashura alimtuliza. “Nipe sababu ya kutoondoka!” mama Ticha alihoji. “Taratibu kwanza!” mama Ashura alisema akimtuliza mama Ticha. “Hebu anza mkanda mwanzo. Ulivyopokea simu alisemaje huyo mwanamke ‘ata akakutia mipresha namna hiyo?” mama Ashura alisema kwa upole.

Mama Ticha akashusha pumzi.

“Aya, anza mwanzo!” mama Ashura alisema.

“Simu iliita. Nikaipokea. Ile kupokea, nikapokelewa na sauti ya bashasha,” mama Ticha alisema akatua. “Sauti ya bashasha hiyo vipi?” mama Ashura alihoji. Akatulia tena mama Ticha. Akaanza kuelezea. “Nilivyopokea, mwanamke akasema.”

“Helo, darling! Uko poa?” sauti kutoka katika simu. “Ukafanyaje sasa?” mama Ashura alisema. “Nikasonya bongwe la sonyo. Nikashushia na neno ‘malaya mkubwa we’” mama Ticha alisema. “He!” mama Ashura alishtuka. “Unashtuka nini sasa?” mama Ticha alisema.

“Mtu hajaongeza neno la tatu, we’ ushaua?” mama Ashura alisema akicheka. “N’shajua yule ni mwanamke wake,” mama Ticha alifura. “We’ umejuaje?” mama Ashura alihoji. “Mume alienda kuoga, aliniambia kama anatoka kuna jambo la kikazi analifuatilia. Sa’ hapo n’tahitaji digrii kujuwa kama napigwa au?” mama Ticha aliwaka.

“Mmmh! Mazito!” mama Ashura alisema.

“Tena sio kidogo!” mama Ticha alisema. Kisha akaonekana kama anabawabu jambo hivi. Akasema. “Panga yuko wapi?” mama Ashura akashtuka. Akamtazama vyema kabisa. “Nd’o unataka kumwaga ugali?” mama Ashura alisema.

“Hapana! Ninataka kumuona tu! Nimemlisi,” mama Ticha alijibu. “Leo hiyo tena?” mama Ashura alisema. “Wacha leja. Nipeleke chumbani kwake. Usiniache peke’angu. Atanibaka!” mama Ticha alisema akiangua kicheko. “Akubake hiyo kwiyo? Na mtu umeenda mwenyewe!” mama Ashura alisema. Wakacheka.

Wakatoka nje hadi mlangoni kwa Panga. Wakagonga mlango. Panga akatoka na rimoti mkononi. Akachanua tabasamu. “Karibuni!” Panga alisema. Hawakuvunga. Wakaingia ndani. Panga hana kiti ndani mwake. Ana ndoo ndogo za maji mbili na kubwa moja kwa ajili ya maji ya kunywa.

Wageni waliendelea kusimama. Akawaribisha kitandani. Wakakubali. Mama Ashura akakaa karibu na Panga. Akajibadilisha. Akamweka mama Ticha karibu na Panga. Wakacheka wote. Kimya kikatawala. Panga rimoti bado ingali mkononi.

“Karibuni sana. Karibuni mno!” Panga aliongeza. Akachanua tena tabasamu. Wale wakajichekesha huku mama Ticha akijibanza katika bega la mama Ashura. Punde, mama Ashura akasikia sauti ya mumewe inamwita. Akaitikia. “Beee! Niko huku!” aliitikia mama Ashura. Akainuka upesiupesi. “Nakuja, mume wangu!” alisema mama Ashura akikimbia. Dirisha likabaki la watu wawili. “Usiondoke nakuja!” alisema mama Ashura angali yuko mlangoni.

Mama Ticha asijibu kitu. Panga akaanza kujichekesha. Akajisogeza zaidi alipo mama Ticha. Mama wa watu hakusogea hata hatua moja. Alibaki kama kabandikwa pale alipo. Panga akanyoosha mkono hadi katika paja la mama Ticha. Akasikia msisimko wa hatari.

Hakuridhika.

Akaanza kusafiri maungoni.

Nani anaweza kuhimili vishindo?

Yakawashinda wote wawili.

Amri ya sita ikavunjwa. Amri maarufu kuliko zote. Amri inayojulikana na vijana na wazee wengi.

Hawakuwa na muda wa kujibaraguzwa. Mama Ticha alivaa nguo zake upesi-upesi na kusogea kando kidogo. Mama Ashura akarudi. Nyuso zao zilikuwa za ukimya, lakini zilitawaliwa na uaibu fulani hivi. Haikuwezekana kujificha mbele ya mama Ashura!

“Aaaaiii... nyinyi!” mama Ashura alisema kwa mshangao.

“Nini tena na wewe?” mama Ticha alidakia. “Kama kuku eeh? Da’ika moja tu kuwaacha, mshalambazana?” mama Ashura alistaajabu. “Mbona hakuna kilichotokea?” mama Ticha alivunga. “Thubutu yako! Jinsi ulivyokuja na hasira... usiniulie mdogo wangu tu!” mama Ashura alisema. Akacheke! Akamtazama Panga usoni. *Akamdindishia*. Hakugeza sura. Panga akashindwa kukaza sura mbele ya mama Ashura. Naye akacheke.

“Kiko wapi!” mama Ashura alisema – baada ya kuona Panga kalitoa cheko la kukubali kuitenda dhambi. Akacheke tena. “Kiko wapi nini wewe?” Panga hatimaye akatoa neno. “Goma sekunde tu nimekuachia, ushalilamba! Loh! Hufai!” mama Ashura alisema. Wakacheke wote watatu.

Mama Ticha akajiweka vyema. “Sasa basi mwambie mdogo wako. Kesho kazi kamili saa nne asubuhi tukutane Lumecha Bar. Yomboooo! Nikauwe mtu!” mama Ticha alitamba. “Mtajuana wenyewe na balaa lenu! Ptuu!” mama Ashura alijibu. Panga katulia. Alikuwa akisikiliza kwa makini.

## SEHEMU YA TATU

**B**uguruni sokoni, majira ya saa kumi jioni. Lori lililosheheni mizigo ya vitunguu na nyanya kutoka mji kasoro bahari—Morogoro—lilikuwa likichekechwa ili liegeshwe. Wakati likiwekwa sawa, kelele na mbinja zilisikika bila kusimama. Lori lilikuwa likitoa moshi mwingi—kiasi ukafanya eneo lililokuwa likijiweka sawa likawa limetawaliwa na moshi uliokithiri.

“Sozigwa! Sozigwa! Sozigwa!” kelele ziliendelea kupigwa hadi hapo gari lilipokaa sawa. Mlango ulifunguliwa, dereva akashuka. Kapelo kaishusha mpaka pajini, macho kayawekea ukuta hasa. Akaiweka sawa kapelo yake kisha akasukuma hatua zake kuelekea katika ofisi ya soko. Njiani vijana walimlaki kwa bashasha huku wakimpiga mabegani.

“Ticha Sozigwa mwenyewe ndani ya nyumba!” tambo zilisikika kutoka kwa kijana mmoja aliyekuwa kando ya Ticha. “Mkubwa Sozigwa, goma limekukubali mwanangu!” kijana aliendelea kumnadi Ticha. “Si unajua tena sisi wengine wandewa anga hizi—ha ha ha ha,” Ticha alitamba.

Alifika katika ofisi ya mkuu wa soko.

“Mkuu, salaam!” Sozigwa alitoa salamu kwa mkuu wa soko. “Salama tu, Sozigwa. Umekuja na nini leo?” mkuu aliitikia salamu na kuuliza msingi wa ujio wa Ticha—ambaye sokoni Buguruni hutambulika kama Sozigwa. “Leo bwana mwendo wa kitunguu na nyanya. Si unajua mizigo ya taifa hiyo kutoka Morogoro,” Ticha alijibu. Akaendelea na taratibu nyingine kabla ya kurudi katika gari na kuchukuwa mkungu wa ndizi uliokuwa umewekwa nyuma ya kiti cha dereva.

Akatazama kulia, kushoto.

Akaitisha bodaboda, limchukuwe apelekwe Kiwalani akiwa na mkungu wake wa ndizi. “Nipeleke Kwa Biti Mussa—Kiwalani,” Ticha alisema. Bodaboda akageuza pikipiki yake, akaiweka usawa wa Sozigwa, safari ikaanza. “Oya! Ayubu, usisahau kuniletea mkaa wangu nyumbani!” Ticha aliongeza. Ayubu ni kijana wake katika gari.

Si Ticha wala bodaboda, wote waliazimia kukata kalima. Mwendo wa kimya mpaka walipofika Kiwalani Minazi Mirefu – upande wa kwa Biti Mussa, Mtaa Maarufu wa Magengeni. Huu ni mji wa mjombaye Ticha. Mjombaye ndiye aliyemlea tangu yungali kijana wa makamo. Ujio wake ukazua furaha kwa familia yake. Kaka amerudi!

Alikuta nduguze kutoka upande wa mjombaye wakiwa kibarazani wameketi wakitazama ya walimwengu yakiendelea. Mjombaye alikuwa juu ya kibaraza na kiti chake cha kulala. Kiti chenye turubai katikati. Hivi ni aina pendwa ya viti kwa watu wa kanda ya pwani.

Akashusha mzigo, akaukabidhi kwa dada zake binamu. Watoto wake wakamlaki baba’o – basi almuradi shangwe baba karudi. Akaachana na mabinamu na watoto wake, akaelekea mahali alipo mjombaye.

“Naona chuma kimerudi,” mjomba alisema akitoa tabasamu.

“Ankoooo!” Ticha alichagiza salamu ya mjombaye. Akamkumbatia mjombaye kisha akaketi kando yake.

“Pole na safari!” mjomba alisema akijiweka sawa kumtazama mwanasafari. “Aaah, huko salama. Sema tu, *trafiki* wanasumbua sana gari za mizigo aina yetu. Karibia kila sehemu tulisimama,” Ticha alisema.

“Nd’o ukubwa huo, mjomba. Ulidhani mambo ni mepesi kama zamani? Dunia imebadilika, na wewe jibadilishe uendane nayo!” mjomba alimsihi Ticha. “Ni kweli anko, lakini hii sasa imekuwa *too much!* Kila sehemu tutowe pesa, kweli?” Ticha alilaani.

“Poleni sana watafutaji. Mi’ nishajizeeka zangu sasa hapa nakula pensheni. Nikikumbuka nyakati zangu nipo BP sikuwa na laza damu. Si unaona majumba haya nimejenga, nina mashamba. Nikiwa kijana sijatoa fursa ya kulalamika – zaidi nilipambana na kila kikwazo kilichokuwapo mbele yangu. Huo ndiyo uanaume!” mjomba aligongomea msumari wa moto.

“Nimekuelewa, anko. Ahsante sana!” Ticha alijibu kinyonge. Akasimama. “Kapumzike mjomba!” mjomba aliongeza. Ticha akaongoza njia kuelekea chumbani kwake. Nyumba ya mzee Kondo, mjombaye Ticha,



ina vyumba vingi sana. Kama ilivyo katika nyumba nyingi za watu wa pwani, ndugu chungutele wamejazana katika kaya ya mzee Kondo.

Wengine hukaa hadi kuolewa au kuoa ndiyo waondoke. Kwa kesi ya Ticha, aligombana na mkewe huko nyuma kwa kushikana ugoni. Mke alimtumumu mume mzinzi sana, mume naye alisema mkewe anamletea maradhi ndani. Wakasemana vibaya manusura waitiane vidole vya macho. Mke wa Ticha alizaa mtoto, Ticha akamkataa kwamba si damu yake. Kwamba damu yake ni kali mno – haiwezekani azaliwe mtoto mpya na asifanane naye. Mtoto sura ya mama. Sijui ni nani aliyempa sumu ya kimamlaka ya kumwambia Ticha kwamba mwanamke ana mashine ya nakala kivuli? Kwa hoja zisizo na kichwa wala mguu, malumbano makubwa yakatokea. Hali ambayo ilimleta kama mkosi ndani ya nyumba.

Baadaye maelewano kukawa hakuna. Si mume wala mke aliyekuwa na uthubutu wa kumsikiliza mwenzake. Mtoto akaanza kuumwa. Mara kifua, mara degedege, mara kaanguka – basi tafrani mtindo mmoja. Hatimaye mtoto asiye na hatia akaondoka katika uso wa dunia. Akawaacha mahayawani wawili waendeleo kulumbana vizuri.

Alivyo mshenzi, hakuthutbu kushiriki mazishi.

Ticha hakuwa mshabiki wa usemi wa *'kitanda hakizai haramu!* Hakutaka kusikia usemi huo. Zaidi aliubatiza jina la *'usemi wa kizembe'* - au *'mhenga mchovu!* Kutoka kwa uhai kwa mtoto, ukawa ndiyo mwisho wa ndoa ya Ticha na mkewe. Mke akamsusia wanawe na kuondoka zake kusikojulikana.

Wakagawana cha kugawa, maisha ya Ticha yakawa ya ovyo sana. Wakati kazi alikuwa hana. Mke alikuwa akifanya kazi katika kampuni ya vinywaji iliyopo Vingunguti. Hofu yake ilikuwa kwamba huyo mtoto ni zao la *godown*. Walivyoachana, mke akaondoka, Ticha akabaki na njaa yake.

Mjomba, ambaye kipindi hicho alijaribu sana kusuluhisha, akamchukuwa mjombaye na kumpatia chumba cha uani, watoto wake nao wakajumuika na wajukuu wengine waliokuwamo wakiishi na babu yao

mzee Kondo. Maisha yakaendelea. Mungu si athumani, Ticha akapata kazi kwa rafiki wa mjombaye anaye miliki malori makubwa ya safari.

Akaitwa na kupewa gari bila kupitia misingi ya awali, yaani, kufanyiwa usaili na uongozi. Kadi ya mjomba ilitumika vyema kumpatia kazi. Ticha akaona huu ndio muda mwafaka wa kurejesha fadhila kwa mjomba. Mzee Kondo ana watoto wa kike wengi kuliko wa kiume. Wa kiume mmoja tu kati ya watoto wa kike watatu. Hatari lakini salama!

Katika watoto wake wa kike, mmoja aliolewa Mafia, ambaye ndiye mkubwa anaitwa Mariam Kondo. Yeye na mumewe walirudi Dar es Salaam wakitokea Mafia ambapo mumewe Mariam alikuwa akifanya kazi. Kazi zilikoma, mume na mke wakarudi nyumbani. Wakafikia ukweni. Akatimiza usemi kamili wa watoto wa mjini, kaolewa badala ya kuo!

Ticha akajenga ukaribu na Mariam, hali ambayo ilipelekea mpaka mumewe aanze kujisikia vibaya. Hebu vuta picha, huna kazi, mkeo anakwambia turudi nyumbani kwa baba, tukaishi maisha yetu. Nyumbani tutakula, tutalala, baba ana uwezo. Twaib! Maalim Kondo ana majumba mengi tu.

Ni kweli watakula, watalala, lakini mpaka lini? Kengele ya hofu ya kuibiwa mke na kaka binamu, mume wa Mariam ikalia. Ililia kwa sauti kubwa mno. Hadhari ya kujinasua mikononi mwa papa mtu ilimuhusu.

“Jamani eh, unajua tangu kakaye binamu Mariam arudi pale ukweni— sielewi kabisa mchongo wao. Naona kama vile anataka kunipiga bao!” alisema mume wa Mariam— mwenye jina maarufu Kiwiko.

“Mbona una wasiwasi sana?” jamaa mmoja kijiweni alimwuliza Kiwiko. “Kazi yenyewe sina. Kazi ya kuchonga maua ya vitanda si kazi. Mpaka upate dili, tayari mke atakuwa keshachukuliwa,” Kiwiko alisema kwa masikitiko.

“Usihofu sana. Mbona hakuna kitakachotokea?” jamaa alirudia tena kumtuliza rafiki yao. Kadiri muda ulivyokuwa unakwenda, ndipo hofu na moyo wa Kiwiko ulizidi kujaa kiza. Wingu la wivu lilitanda moyoni mwake.

Ticha kila akirudi safari alikuwa akimletea zawadi Mariam. Ukaribu ukafikia hadi kupikiana chakula wakati akirudi.

“We’ mtoto ujuwe utanipa tu. Nataka kurudisha fadhila kwa mzee. Amenisitiri nyumbani kwake, amenitafutia kazi. Nataka nini tena? Bora mali zisiende mbali!” Ticha alijinadi mbele ya Mariam Kondo. “Si unajua kama nina mume lakini au unajitia wazimu tu?” Mariam alijibu akimtazama Ticha.

“Yule mume au jina tu? Mume hana pesa, hatafuti pesa, wala hazijuwi ziko wapi. Yeye kang’ang’ania uselemara kama ana udugu nao vile,” Ticha alichagiza. “Eeeh, babu eh em mpunzishe mume wangu. Kakukosea nini?” Mariam aliwaka. Ticha akacheka.

Wakati maongezi haya yakiendelea, Ticha aliketi kando ya Mariam aliyekuwa akisonga ugali jikoni kwao uani. Moshi wa kuni haukumshughulisha Ticha maadamu alikuwa na dhamira ya kutimiza jambo lake. “Sasa ninakwambia, tena unisikize kwa uzuri. Ninaenda safari hii Morogoro, nikirudi wewe utanipa nitakacho mwenyewe!” Ticha alisema kwa msisitizo. Uso wake ulikuwa hautanii. Mariam akacheka kwa kuamini hakuna kitakachotokea.

\*\*\*\*\*

Miezi mitatu baadaye, Ticha alirudi safarini na kuku wa kubanikwa mkononi. Kama kawaida yake, alitoa salamu kwa watu wote baadaye akatafuta muda wa pekee kwa ajili ya Mariam. Dada yake binamu. Dada yake aliyesema hatothubutu kula nyama ya hamu. Leo imeletwa! “Mariam!” Ticha aliita kwa sauti. Mariam akatoka chumbani kwake, khanga kifuni. “Unasemaje we msafiri – kelele mtindo mmoja!” Mariam alisema. Kabla ya kuvuka kizingiti cha mlango wa chumbani kwake, mumewe akatokea kwa nyuma. Akamtolea salamu Ticha. Lakini uso aliufinyanga. Kisirani moto!

Salamu Ticha akazipata. Kwamba bwana kaka hapendi uhusiano wao. Hakujali. Ticha aliamini mume wa Mariam ni marioo tu. Anasaidiwa ukweni. Hana maajabu wala jipya. Mbele yake, akasema.

“Nimekuletea zawadi mama watoto!” Ticha alisema akinyoosha mkono. Akamkabidhi Mariam kuku aliyebanikwa kwa ustadi mkubwa. Kabla ya kufunuliwa, hupata salamu ya harufu ya viungo. Akampokea kisha akageuka nyuma kumtazama mumewe.

Ndita zilienea usoni pote pa mume wa Mariam.

Mariam akajichekesha. “Aya – ahsante!” Mariam alisema akirudi chumbani. Ticha kwa aibu, akaondoka na yeye. Mariam akapika ugali, akala kuku. Mumewe akakataa kula nyama hiyo. Mariam hakujali. Akaikung’uta mpaka mfupa wa mwisho. Tangu ale nyama ya Ticha, akili zake zikaanza kwenda arijojo. Polepole akajikuta anaingia moyoni kwa Ticha bila kupenda.

“We’ mwanaume, inakuwaje nahisi kukupenda-penda?” Mariam alisema kwa njia ya simu. Alimpigia Ticha aliyekuwa safarini.

“Nilikwambia Mariam. Nikirudi safari umekwisha. Nilivyokupa kuku, sikutarajia kama ungemla. Sasa mimi na wewe ndiyo tushakuwa wapenzi. Kataa kama unaweza!” Ticha alitamba.

Mariam akatahayari. Akitafakari ni kweli kuku kala. Hisia za kimapenzi ni kweli zinamjia juu ya Ticha. Ulozi umeuhusika!

“Mungu wangu! Nimefanya nini mimi?” Mariam alijuta nafsini. “Nilidhani anatania kumbe yuko *serious*? Tobaa!” Mariam aliendelea kujiuliza mikono ingali kichwani.

Kadiri muda ulivyokwenda, ndivyo Mariam alivyozidi kuzama katika kisima cha huba ulozi la Ticha. Mumewe Mariam akahamia katika ulimwengu wa pombe. Akawa mtu wa kunywa kila wakati. Pombe zikapelekea aanze kupoteza nuru yake ya kuvutia. Akawa anatafakari jinsi alivyopasua ukuta wa Mariam kwa mara ya kwanza.

Akamwahidi kumpenda mpaka milele.

Ahadi yenye kalima ‘dumu dawamu!’

Ahadi ambayo imeingiliwa na fisimtu.

Akawa analala nje. Akinywa, hachagui pa kukaa wala kulala. Popote pombe zitakapomwanguka, basi hukuruza usingizi na asiwe na wasiwasi. Hatimaye Mariam na Ticha wakawa wapenzi. Kukawa hakuna siri. Mjomba

aliwaka mpaka dakika ya mwisho, lakini Mariam tayari alikuwa mtu mzima. Si rahisi tena kumtawala.

Akamtimua Ticha nyumbani kwake kwa kumfedhehesha. Kwa kumgombanisha na mkwewe. Mariam na mumewe wakaachana rasmi. Mariam akahamia nyumbani kwa Ticha huko Temeke ABC – kwa mama Said. Wakaishi kama mume na mke kabla ya ndoa rasmi kutokea hapo baadaye.

Ahadi kubwa aliyoitoa Kiwiko kwa mkewe.

“Mariam mke wangu. Umeamua kutotambua utu wangu kwa sababu ya binamu yako. Itoshe kusema nimevumilia mengi sana. Sasa nimefika ukingoni. Ahadi yangu kwako ni moja tu. Hutoishi maisha ya furaha kamwe.

Hutofurahia utamu wa ndoa yako haramu na huyo mwanaharamu mwenzako. Nitahakikisha ninaichukua furaha yako kwa hali na mali! Kila la shari likufike huko uendako,” Kiwiko alisema akikabidhi talaka kwa Mariam. Shingo upande. Akili na macho yanakataa kuona mkono ukinyoosha kutoa talaka.

Mke pekee. Hakuwahi kufanya jambo lolote kwa mkewe huko nyuma. Aliamini katika mapenzi. Alimchukuwa Mariam akiwa mwanamwali. Hakuamini wakati huo, na sasa haamini kama kweli anatoa talaka. Anamkabidhi bucha fisi. Ikawa ndoa imekufa rasmi. Japo Mariam hakusubiri talaka ili aishi na Ticha kama mume.

Kwa kinyongo, mzee Kondo akaruhusu bintiye aolewe na mtoto wa dadaye. Ndoa ikafungwa na beni-bati likapigwa. Baada ya upepo wa kusi kupoa, Mariam na Ticha wakahamia Kiwalani Chadema. Miaka ikakatika tangu ndoa itukie. Mume akawa ana hamu ya kupata mtoto na binamu yake. Binamu mambo yameenda arijojo.

“Unajua sikuelewi, Mariam – inakuwaje kila siku nalilia mtoto na sipati? Acha kula vidonge!” Ticha aliwaka.

Picha limeanza!

Mariam akaanza kujihangaisha mashariki na magharibi, kusini kwa kaskazini. Hola! Anamtafuta mchawi. Shika mimba, mimba shika na wewe. Hakuna mimba wala mtoto wa mimba. Hakuwahipo kula vidonge vya majira. Hakuwahipo kufunga kizazi kwa vipini wala njia yoyote inayohusu *nyota ya kijani*.

Ticha akawa mtu wa masimango. Anataka mtoto wa nguvu zote kiasi hata kusahau utu wa Mariam. “Sasa kama umeshindwa kunizalia, nakutafutia mtoto nje—nitakuletea ulee. Maana wewe mayai yako umekaangia chips!” Ticha alisema huku akimtia masingi Mariam. Ticha akaanza rasmi kutembea na wanawake nje. Kila siku meseji ya mwanamke yule mara harudi nyumbani kabisa. Basi tafrani kila iitwayo leo.

Furaha ya ndoa ikamwingia nyongo. Uchungu, uchungu kila uchao. Mariam anaishi na Ticha kwa shinikizo la babaye kwa vile aliitaka mwenyewe ndoa na Ticha. Mariam akakosa msaada. Kila akienda kulia kwao, anafukuzwa. Siku moja akiwa kibarazani kwao, akapokea ugeni wa mama Ashura. Mama Ashura akamweleza kuhusu Panga.

Salamu hizi hakuzifikiria mara mbili. Alijua sasa umefika wakati wa kumchimba kobe. Keshakaa katika mkao wake. Gamba lake limetiwa kijiti, shingo haizami tena. Masimango kila siku, mume mtu wa gubu kama ndugu wa mume—kumbe mume ndiye yeye.

Wakati akiwa katika tafakuri juu ya uamuzi wake aidha amkubalie Panga au amkatalie, akakumbana na simu ya msichana aliyekuwa akimwuliza mumewe yu wapi.

Uamuzi uliofikiwa kila mmoja afanye yake. Mume kamwaga mboga, Mariam akamwaga ugali. Mariam na Panga, Ticha na wanawake wengine nje. Kama mbwai, mbwai!

**SEHEMU YA NNE**

“**D**ah! Si mchezo! Kweli umejuwa kukonga mtima wangu!” Mariam alisema huku akisindikiza na busu shavuni kwa Panga. Mwendo wa ngiri, jino nje.

“Nimemuweza, mshenzi huyu! Mtoto mtamu mpaka basi!” Panga aliwaza nafsi. Akamtazama Mariam kisha akatabasamu.

“Kipi kilichopelekea kuzaliwa kwa hilo tabasamu lako?” Mariam aliuliza huku akimgusa mwamba wa pua wa Panga. “Hamna kitu, mpenzi. Kawaida tu!” Panga alijibu. Mariam akajitoa maungoni mwa Panga. Akaenda pochi yake ilikuwako juu ya meza. Zile panda shuka za maungo ya Mariam zilitikisa hisia za Panga kupita maelezo.

Akatoa kiboksi kidogo. Ndani yake kulikuwa na karatasi imefinyangwa. Katika hali isiyo ya kawaida, Mariam akamtupia jicho la huba Panga. Jicho ambalo Panga hakuwahipo kuliona. Panga moyo ukaanza kumwenda mbio. Hakuamini kilichokuwa kikitokea ndani ya chumba nambari ishirini na tano – ndani ya Kaundime Lodge.

Mariam alishika pete. Pete ndogo ya kidole. Alinyoosha mkono na kumpa Panga.

“Nivishe hii pete!” Mariam alisema akimkabidhi Panga aishike. Panga kiwewe. Moyo wake ulitamani kutoka katika mwili wake. Mdundo ambao mishipa inayoushika ilijua kupata mateso. Maana haukuwa mdundo wa kitoto.

“Pete?” Panga alimaka.

“Mbona sikuelewi?” Panga aliongeza. “Sasa huelewi kitu gani? Hiyo ni pete. Nivishe niwe mchumba’ko rasmi!” Afanalek! wallah! Panga mikono kichwani. Chumba alikiona kinatembea. Wakati yungali palepale. “Tafadhali, usinitende. Ninakukabidhi moyo wangu rasmi. Nipende kwa hali yoyote ile!” Mariam alisema akiwa katika huba zito. Hakuelewa hasi wala chanya.

“Mariam!” Panga aliita kwa kihoro.

“Abee, Panga!”

“Hilo haliwezekani!”

“Kwanini?”

“Tayari una mume. Huwezi kuchumbiwa tena.”

“Kwanini hutaki kusikiza hitaji la moyo wangu? Natamani lile jitu lipotelee mbali ili niweze kujifaidia na nimpendae kwa moyo wangu wote!” Mariam alisema kwa masikitiko. Panga hakuwa na uwezo kuunga mkono ajenda ya pete hata kwa nukta moja. Zaidi aliwazia swali la mama Ashura kuhusu utimilifu wa marinda yake. Huenda yakahitajika.

Kiwewe!

“Basi naomba muda kidogo nikajitafakari. Niupime uzito wa jambo lenyewe kisha nitarudi kwako. Sawa, mpenzi?” Panga alisema. Mariam akaitikia kwa shingo upande. Lakini afanyaje? Panga akaingia rasmi katika ulimwengu wa kusokota mawazo. “Mi’ sikufikiria kama atazama kiasi hiki. Nini mwisho wa huba hili?” Panga aliendelea kuwaza na kuwazua.

Wakaachana. Kila mtu alirudi kwake.

“Kuna haja ya kumshirikisha mshenga katika hili,” Panga aliendelea kujiuliza. Pamoja na utukutu wake, katika hili Panga ameshindwa kujitathmini. Akajikuta mlangoni kwa mama Ashura kwa ushauri zaidi.

“Mama Ashura!”

“Mama Ashura!”

Panga aliita kwa kihoro. Moyo ukimwenda mbio. Hajui achaguwe nini kati ya mapendekezo aliyopewa na mama Ticha. Mama Ashura akatokea. “Vipi hivyo kutugongea lango kama mtu kafa?” mama Ashura aliwaka. “Sister!” Panga alisema, akatua. Akameza funda la mate akimtazama mama Ashura.

“Vipi, umekimbizwa na wezi au umefumaniwa?” mama Ashura alihoji. “Bora ingekuwa hivyo,” Panga alisema akihema.

“Shoga’ko!” Panga alisema.

“Kafanyaje? Kafia gesti au?”

“Em tulia basi, mama Ashura!”



“Sema basi kafanyaje huyo shoga’ngu?”

Panga akatulia – na mchecheto juu. Akavuta pumzi – akijaribu kushusha presha ya habari. “Anataka!” Panga alisita tena. “Anataka nini? Kukutoa roho au?” mama Ashura aliwaka tena. “We’ usinipotezee muda wangu,” mama Ashura alisema kwa hamaki. Akafunga mlango wake, lakini Panga akauzuia kwa mkono wake.

“Sema sasa ana nini?” mama Ashura alifoka.

“Pete!” Panga alisema.

“Imefanyaje hiyo pete?”

“Anataka nimvishe pete ya uchumba!”

“Lahaula walakuata!” mama Ashura mikono kichwani. Kichwa akakirudisha ndani. Akaishiwa pozi jumla. Akamtazama Panga usoni. Hakummaliza. Akatoka kabisa nje. Akati anajaribu kuvuka kizingiti, akajikwaa. Panga akamdaka.

“Vipi tena, mama Ashura?” Panga alisema akimdaka mama Ashura. “Mmmh! Mazito!” mama Ashura alisema. “Kwani umempa nini yule mwanamke? Maana hata sijui nianzie wapi!” mama Ashura alisema aking’uta mikono.

“Niambie nifanyaje?” Panga alisema kwa kihoro. “Hata sijuwi mwenzangu. Najionea tabu tu. Halafu...” akayakata maneno yake mama Ashura. “Halafu nini, mama Ashura?” Panga akadakia. “Alikuwa nayo hiyo pete kwangu. Akaniambia *surprise* lakini hakusema ya nani. Sasa hivi unavyoniambia ndiyo nimechoka kabisa. Loh! Yule mwanamke!” mama Ashura aliendelea kusikitika.

“Kwani mnafanyaga nini hata akachanganyikiwa hiv’o?” mama Ashura alihoji. “Viuno vya Buza!” Panga alijibu. Akacheka mwenyewe kwa jibu lake. Mama Ashura naye akasindikiza cheko hilo. Wakawa wanacheka wote kwa pamoja.

“Nd’o ukomege na wewe. Mtoto mdogo unapagawisha watu wazima, matokeo yake nd’o hayo. Haya sasa mtu mzima anaadhirika kwa kutaka kuchumbiwa kwa mara ya pili. We’ unadhani hiyo akili yake hiyo?”

Chezo hilo. Sijui nd’o ulimpa mtindo wa *paka chongo*. Miuno feni bovu miksa ya uzazi!” mama Ashura alisema.

“Aisee! Hata sielewi nifanyeje!” Panga alisema. “Nd’o itabidi umvalishe tu. Japo si kihalali, lakini iwe kama unamridhisha moyo wake. Ila tu,” mama Ashura akakata maneno yake. Ni baada ya kumuona msichana mrembo kwa mbali mwenye umbo nambari nane, dimpozi zimezama, rangi ya chokleti na mwendo wa twigwa akiwasili.

Usowe ulipambwa vyema na tabasamu mwanana. Meno yake meupe pee, mwenye kimo cha mgongo wa chura, kishungi kimetoka kwa nyuma. Alisogea hadi walipo akina Panga na mama Ashura.

“Bwawa limeingia ruba!” alisema mama Ashura. Panga akageuka. Hamadi! Mwanamke wake aliyesafiri kwenda Arusha kikazi, amerudi!

“Baaabbbyyy!” huyo msichana aliita kwa bashasha huku akimkimbilia mpenziwe Panga. “Jamila!” Panga alisema kwa mshituko. Hakuamini macho yake. Muda wa majibu anapata maswali. Panga mwenye unyonge wa nafsi kutokana na penzi la mama Ticha, akajikuta anashindwa kumpokea kwa furaha mpenziwe. Akaumba tabasamu bandia akimkimbilia Jamila.

“Baby, vipi? Mbona kama hauko sawa?” Jamila alimwuliza Panga. “Baby, we acha tu. Ni mambo ya dunia!” Panga alijibu. Jamila akajitoa maungoni mwa Panga. Akarudi nyuma hatua moja. Akamtazama mpezi wake usoni. Akainua kidole cha shahada hadi kidevuni mwa Panga.

Akakiinua kichwa chake. “Naomba unitazame mpenzi,” Jamila alisema. “Nini mbaya, baba’ngu?” Jamila aliongeza. Alitoa sauti ya huba. Sauti ya kusimamisha injini ya meli pindi isikiapo sauti hiyo. Jicho basi alilokuwa akimrembulia Panga, halisemezeki.

Mama Ashura aliutazama mchezo wote. Alijua fika mdogo wake yamemkuta ya kumkuta mwaka huu. “Pole sana, Panga!” mama Ashura alisema akicheka na kuondoka. Panga akamchukua Jamila hadi chumbani kwake.

Wakaketi wote kitandani. Jamila akatoa maungoni mwake kiblauzi chake cha rangi ya nyeusi. Alivaa na suruali ya jinzi buluu, kiatu mchuchumio. Akasaula kila kitu, akaendea mkoba wake ulipo, akatoa khanga, akajifunga kifuani.

“Haya, niambie sasa nini kinakutesa moyo wako?”

\*\*\*\*\*

Uhusiano wa Panga na Jamila ulianza miezi nane iliyopita – kabla ya safari yake ya kwenda Arusha kikazi. Hakukuwa na barua wala simu. Jamila alipotea jumla. Ilikuwa eneo maarufu la kwa mama Teddy – Kiwalani Minazi Mirefu. Eneo la watoto wa mjini wenye visanga vyao. Wenye kutikisa Kiwalani yao kwa uchezaji wao wa ‘bikini chali.’

Jamila na Panga walikutana kwa fundi nguo maarufu fundi Madenge. Fundi wa miaka mingi Kiwalani. Mjuvi wa mavazi yote ya kushonesha. Panga alileta shati lake kupunguzwa ukubwa. Jamila alileta kitambaa ashonewe gauni refu mpaka miguuni.

Macho ya uchu ya Panga yalipotua juu ya bolibo za Jamila, akaingia tamaa. Ulimi ukamponyoka. Kutokana na kutofautiana hatua, Panga akamsogelea Jamila alipo. Karibu kabisa na fundi Madenge.

“Mrembo, uhali gani?” Panga lilimtoka neno. Jamila akabaki kimya. Asijibu lolote. “Mrembo hujambo?” Panga aliongeza. Jamila akashangaa, “Unanisalimia miye au?” Jamila alihoji ilhali pale alipo dada alikuwa yeye pekee. Hali iliyopelekea fundi Madenge atoe tabasamu hafifu.

“Ni wewe pekee, mrembo! Hakunaga mwingine kama wewe!” Panga alijibu kwa tashtiti. Jamila akacheka. Madenge akasonya. “Ushaanza balaa lako tena we’ mtoto ulokosa radhi!” Madenge alifoka akicheka. “Tulia basi Madenge. Utakosa kura yangu katika uenyekiti wako!” Panga alimtania Madenge.

Wakacheka kwa pamoja.

“Binti, kuwa makini. Firauni huyo kama kitu gani vile!” Madenge aliendelea kuharibu. Lakini maneno yake hayakuweza kuyeyusha

tabasamu la Jamila kwa Panga. “Usimsikize huyu. Anazingua tu!” Panga alijitetea.

“Usijali!” Jamila alijibu akiweka kidole cha shahada mdomoni. Akakibana kwa papi za midomo yake. Panga akapangika. Mkono akautoa, “Naomba nikusalimie!” Panga alisema huku akinyoosha mkono. Jamila hakumfanyia hiyana. Akanyoosha mkono, akampatia.

“Umeridhika?” Jamila alihoji. Mambo aliyokuwa akiyapitia baada ya kushika mkono wa Jamila yalikuwa hayasemezeki. Mwili ulipigwa ganzi ya umeme. Alijihisi hana mamlaka na mwili wake. Panga akatwaliwa na sura ya huruma.

“Vipi tena, kaka?” Jamila alisema. Ni baada ya kumuona Panga kazubaa. “Sikutegemea kama kweli malaika wapo! Tena hapa duniani!” Panga alisema huku akibadili sura yake kuzidi kuwa ya huba badala ya kutia huruma. Madenge akatabasamu.

“Anaibiwa mtu!” Madenge aliropoka. “Em tulia basi na we’ mzee!” Panga aliwaka. Madenge akaporomoshia cheko la kufa mtu. “Tokeni nje mkaongee. Msinitilie nuksi ofisini kwangu!” Madenge alikoleza sumu ya nongwa. Panga akamtazama Jamila. Hakujibu kitu baada ya mistari yake konzi. “Fundi tumemalizana?” Jamila alisema akimtumbulia macho fundi.

“Nafikiri kilichobaki ni kunipa *advance* yangu tu. Uje uchukuwe gauni lako baada ya wiki!” Madenge alisema. Jamila akatoa noti ya shilingi elfu tano na kumkabidhi fundi Madenge. “Aya, ahsante eh!” Jamila alishukuru akitoka nje. Panga akamwunganishia.

“Nyoo! Utakufa!” Madenge alimshambulia Panga. Panga masikio aliziba pamba. “Tulia we’ kibanizi...” aliyakata maneno yake kwa kumkimbilia Jamila. “Samahani, dada! Samahani!” Panga alisema akimvuta mkono Jamila. Akavuta pumzi kidogo.

“Unajua hatujatambulishana rasmi. Mimi ninaitwa Hassan Kiroboto – jina maarufu Panga la Mwingereza. Marafiki zangu wanalifupisha na kuniita Panga!” Akavuta ukimya kwa nukta kadhaa kisha akaendelea.

“Je, mwenzangu unaitwa nani na unakaa wapi?” Panga akatua kalima. Jamila akawa anajibaraguzwa. “Um, mi’ naitwa Jamila. Ninaishi hapo nyuma tu kwa Mwakalinga,” Jamila alisema akifungua safari ya kurudi kwao. Panga akamzuia kwa mbele.

“Nisingependa niwe mtumiaji wa muda wako. Vilevile nisingependa tuongee wima mithili ya *askari kea*,” akasita kuendelea kuongea Panga. Akamkagua Jamila kuanzia chini mpaka juu. “Una vitu vyote anavyohitaji kuwa navyo mwanamke,” Panga alitua.

Jamila akacheka.

“Nikusaidieje?” Jamila alisema.

“Naomba namba yako tu. Moyo wangu utakuwa umeukonga jumla!” Panga alisema akijinyongesha. “Sawa. Nipe simu yako nikuandikie,” Jamila alisema akinyoosha mkono apokee simu. Panga hakujivunga. Akaitoa simu, na kumkabidhi Jamila.

“Kiswaswadu!” Jamila alisema akicheka. Ni baada ya kuiona simu ya Panga. Simu ya tochi. “Ah, *smart* hizo tunaawachia warembo bwana! Asili ya kazi zetu ni ngumu kuwa na *smart*. M’da wowote unalia! Ya nini kuumia wakati humu maisha yanaendelea?” Panga alijitetea.

“Usijali!” alisema Jamila kwa lafudhi za watoto wa kike wanajuwa kuwaingiza vijana wa rika lao mtegoni mwao. Usijali yenye lafudhi ya ‘R’ badala ya ‘L.’ Jamila akaandika namba, wakaachana. Baadaye wakawa na mawasiliano mazuri na hatimaye wakawa wapenzi kwa wiki tatu, baadaye Jamila akaenda Arusha kikazi.

Alikuwa anafanya kazi katika kampuni ya kitalii. Hasa alikuwa kama msimamizi wa masuala ya usafi na kuwasimamia wafanyakazi waliokuwa wakifanyia watalii masaji. Jamila na Panga walitengeneza jozi thabiti la wapenzi.